**BENKI KUU YA TANZANIA**

# MWONGOZO WA NAMNA YA KUSHIRIKI KATIKA SOKO LA AWALI NA LA UPILI LA DHAMANA ZA SERIKALI ZA MUDA MFUPI

© 2022

## SOKO LA DHAMANA ZA SERIKALI ZA MUDA MFUPI

### 1.1 UTANGULIZI

Benki Kuu ya Tanzania kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, huuza Dhamana za Serikali ikiwa ni njia ya kukopa fedha kutoka kwa taasisi ama mwananchi mmoja mmoja.

Dhamana za Serikali za muda mfupi ni Dhamana zinazoiva katika muda usiozidi mwaka mmoja. Dhamana za Serikali za muda mfupi kwa kiwango kikubwa huiwezesha Serikali kugharamia nakisi katika bajeti yake inayosababishwa na upungufu wa mapato ukilinganisha na matumizi ya Serikali.

Dhamana za Serikali huuzwa kwenye soko la awali kwa njia ya ushindani kupitia minada na baada ya hapo uuzaji wa Dhamana hizo hufanywa kwenye soko la upili.

Ununuzi wa Dhamana za Serikali ikiwa ni njia mojawapo

ya uwekezaji ina faida zifuatazo:

- Kuwekeza katika Dhamana za Serikali ni salama kwani Serikali haitarajiwi kukiuka mategemeo ya wadai wake wakati wa malipo.
- Dhamana za Serikali zinahamishika, hivyo mwekezaji anaweza kuziuza kabla ya muda wake wa kuiva endapo itakuwa ni lazima afanye hivyo.
- Dhamana za Serikali zinaweza kutolewa kama Dhamana kwa ajili ya mkopo.
- Dhamana za Serikali zina kiwango cha faida inayoridhisha.

Mwongozo huu umegawanyika katika sehemu kuu nne, nazo ni mfumo wa soko na namna ya kushiriki, mchakato wa mnada, utaratibu wa malipo na uuzaji wa Dhamana za muda mfupi katika soko la upili.

## 2.0 MFUMO WA SOKO NA NAMNA YA KUSHIRIKI

### 2.1 Mfumo wa Soko

Kuna aina mbili ya Masoko ya Dhamana za Serikali, soko la awali ni pale ambapo Benki Kuu huuza Dhamana za Serikali kwa mara ya kwanza. Mnada hufanyika kila baada ya wiki mbili. Uuzaji wa Dhamana hizo baada ya hapo hufanywa kwenye soko la upili.

### 2.2 Wawekezaji Wanaostahili Kushiriki

Kila mkazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki anastahili kushiriki katika mnada wa Dhamana za Serikali za muda mfupi. Wakala au mwekezaji mwenye kiwango cha kuanzia shilingi laki tano (TZS 500,000.00) na kuendelea anaruhusiwa kushiriki katika mnada wa Dhamana za Serikali za muda mfupi.

### 2.3 Mfumo wa Kuhifadhi Kumbukumbu

Benki Kuu ya Tanzania inao mfumo maalum wa kushughulikia na kuhifadhi taarifa zote za minada ya Dhamana za Serikali za muda mfupi. Minada yote ya Dhamana hizo hufanyika na

kumbukumbu zake huwekwa kwa njia za kielektroniki. Hivyo basi, hakuna shahada au hati inayotolewa kwa wawekezaji.

## 3.0 MCHAKATO WA MNADA NA TARATIBU YA KUTUMA ZABUNI

Benki Kuu ya Tanzania hutoa Dhamana za serikali za muda mfupi na zinazoiva kwa nyakati tofauti. Dhamana hizi ni za siku 35, siku 91, siku 182 na siku 364.

### 3.1 Uitishaji wa Zabuni

Tangazo kupitia vyombo vya habari (ambalo pia litakuwa '***prospectus',*** tazama **kiambatanisho I**) litatolewa wiki moja kabla ya siku ya mnada.

### 3.2 Kuwasilisha Fomu Za Zabuni

Washiriki watapaswa kutumia fomu maalum za zabuni zenye namba **CDS/FORM/III** kwa ajili ya kushiriki katika minada ya Dhamana za Serikali **(kiambatanisho II**). Fomu hizi zitapatikana kwenye tovuti ya Benki Kuu ya Tanzania na katika ofisi za Mawakala waliosajiliwa.

Kiwango cha chini cha kuwekeza kwenye Dhamana za Serikali za muda mfupi ni shilingi laki tano tu (TZS 500,000) zikiwa katika mafungu ya shilingi elfu kumi kumi (TZS10, 000)

Bei ya Dhamana za Serikali za muda mfupi zinapaswa kuwa na tarakimu nne za desimali.

Wawekezaji watawasilisha fomu za zabuni kwa Mawakala waliosajiliwa. Fomu hizo zilizojazwa zikiwa na saini ya mwombaji zinatakiwa ziwasilishwe kwenye ofisi za mawakala waliosajiliwa ambao watazituma Benki Kuu kwa njia ya kielektroniki kupitia kwenye mtandao.

**Benki Kuu ya Tanzania inayo haki ya kukubali au kukataa fomu mojawapo ya zabuni au zote zilizowasilishwa katika mnada husika.**

## 3.3 Mgawanyo Wa Dhamana Zilizotolewa Kwa Wazabuni Walioshinda.

Benki Kuu ya Tanzania huendesha mnada kwa kutumia mfumo wa kieletroniki ujulikanao kama mfumo wa Dhamana za Serikali 'Government Securities System' (GSS). Ili kuwatambua washindi, mfumo wa mnada hutumia mfumo wa bei tofauti. Kila mzabuni aliyeshinda atawajibika kulipia zabuni yake kwa bei aliyopendekeza.

Washindi wa zabuni wataorodheshwa, kwa kuanzia na aliyetoa bei ya juu zaidi hadi yule wa bei ya chini kabisa mpaka pale ambapo mafungu yaliyotolewa kwa ajili ya mauzo ya Dhamana hizo yanamalizika.

Endapo washindi katika bei ya mwisho watahitaji kiwango cha Dhamana zaidi ya kiwango kilichobaki katika mafungu yaliyotolewa, Benki Kuu ya Tanzania itawagawia washindi wote kiasi kilichobaki kwa uwiano wa zabuni zao hadi kiwango kilichobaki kitakapomalizika.

### 3.4 Kutangaza Matokeo Na Kutoa Namba Ya Kutuma Malipo

Matokeo ya mnada yatatangazwa kwenye tovuti ya Benki Kuu ya Tanzania:- https://www.bot.go.tz. Mawakala waliosajiliwa pia watapata matokeo hayo mara tu baada ya mnada.

Wazabuni watakaoshinda watapatiwa namba za malipo kupitia kwa Mawakala mara baada ya matokeo ya mnada kutolewa. Namba hizo za malipo zitatumika kama namba za marejeo kwa ajili ya kufanya malipo ya Dhamana za Serikali zilizonunuliwa kwa kupitia mfumo wa malipo kati ya mabenki, yaani 'Tanzania Interbank Settlement System' (TISS).

## 4.0 MALIPO

### 4.1 Malipo Kwa Washindi Wa Mnada

- Wazabuni walioshinda watapaswa kulipia malipo ya Dhamana walizoshinda katika muda wa siku moja (T+1) baada ya mnada husika kufanyika.
- Wawekezaji wote walioshinda katika mnada watapaswa kufanya malipo kupitia mfumo wa malipo kwa mabenki nchini (TISS), kupitia katika mabenki yaliyosajiriwa na Benki Kuu ya Tanzania.
- Endapo wazabuni walioshinda hawataweza kulipia zabuni zao ndani ya muda uliopangwa, basi watazuiliwa kushiriki katika minada kwa kipindi kisicho pungua mwezi mmoja baada ya mnada alioshindwa kuulipia.

Taarifa inayoonyesha miliki ya Dhamana za Serikali alizonazo muwekezaji itatolewa kila inapohitajika.

## 4.2 Malipo ya mwisho wa kipindi cha uwekezaji

Muda wa kuiva kwa Dhamana za muda mfupi utakapowadia, wawekezaji watalipwa asilimia mia moja ya thamani ya Dhamana ikiwa imejumuisha thamani ya manunuzi na faida.

Benki Kuu ya Tanzania itafanya malipo hayo kwa wawekezaji wote kwa wakati mmoja.Wawekezaji wote watalipwa stahiki zao kupitia akaunti zao katika mabenki.

## 4.3 Kodi ya Zuio

- Mapato yatokanayo na uwekezaji katika Dhamana za Serikali za muda mfupi yatalipiwa kodi kwa mujibu wa taratibu za Serikali zilizopo.
- Wale wawekezaji waliosamehewa kulipa kodi watapaswa kuwasilisha Benki Kuu cheti cha uthibitisho wa msamaha huo kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania.

## 5.0 UUZAJI WA DHAMANA ZA SERIKALI ZA MUDA MFUPI KATIKA SOKO LA UPILI

- Mauzo na manunuzi ya Dhamana za muda mfupi yatafanyika kwa njia ya makubaliano kati ya muuzaji na mnunuzi (Over-The-Counter) na ni baada ya Dhamana hizo kuuzwa katika soko la awali.

- Uhamishaji wa Dhamana za muda mfupi zilizouzwa na wamiliki, baada ya soko la awali utafanywa kwa

  kuhamisha kumbukumbu katika vitabu vya kumbukumbu za wamiliki wa Dhamana za Serikali. Uhamishaji huo wa kumbukumbu, kutoka kwa mmiliki wa zamani na kwenda kwa mmiliki mpya utafanyika kupitia kwa Mawakala wa Dhamana za Serikali (CDPs) kwa kujaza fomu za uhamishaji wa Dhamana "**FOMU ZA BENKI KUU YA TANZANIA ZA KUHAMISHA DHAMANA-TF" (kiambatanisho III).**

- Muuzaji na Mnunuzi wa Dhamana za Serikali, kila mmoja wao atawasilisha fomu za uhamishaji wa Dhamana zilizojazwa sawia kwenye ofisi ya wakala wake

- Wakala atahamisha umiliki wa Dhamana kama kielektoniki kama inavyopaswa.

- Fomu za uhamishaji wa Dhamana za Serikali "**FOMU ZA BENKI KUU YA TANZANIA-TF" CDS/FORM/03 (Kiambatanisho III)** zinapatikana kwenye ofisi za mawakala waliosajiliwa na tovuti ta Benki kuu ya Tanzania:- https:// www.bot.go.tz

- Fomu za uhamishaji wa Dhamana za Serikali "CDS/FORM/05 **(Kiambatanisho IV)** zinapatikana katika tovuti ya Benki Kuu ya Tanzania,

https://www.bot.go.tz na kwenye ofisi za mawakala waliosajiliwa.

- Baada ya muda wa kushikiliwa kwa Dhamana kuwa umekwisha, wawekazaji husika watapaswa kuwakilisha fomu ya kuzirudisha Dhamana kwa mwenye nazo (Lien Release form), **CDS/FORM/06 (Kiambatanisho V)** zinazopatikana katika tovuti ya Benki Kuu ya Tanzaninia na kwenye ofisi za mawakala waliosajiliwa

**MAWAKALA WALIOSAJILIWA:**

Benki Kuu ya Tanzania imesajili mabenki na madali wa soko la Hisa la Dar Es Salaam kufanya kazi za uwakala kwa wawekezaji katika Dhamana za Serikali kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| 1 | ABSA BANK TANZANIA LIMITED |
| 2 | ACCESS BANK TANZANIA LIMITED |
| 3 | AFRICAN BANKING CORPORATION TANZANIA LTD |
| 4 | AKIBA COMMERCIAL BANK LIMITED |
| 5 | AMANA BANK LIMITED |
| 6 | ARCH CO LIMITED |
| 7 | AZANIA BANK LIMITED |
| 8 | BANK OF AFRICA (T) LIMITED |
| 9 | BANK OF BARODA (T) LIMITED |
| 10 | BANK OF INDIA (TANZANIA) LIMITED |
| 11 | CANARA BANK TANZANIA LIMITED |
| 12 | CHINA DASHENG BANK LIMITED |
| 13 | CITIBANK TANZANIA LIMITED |
| 14 | CORE SECURITIES LIMITED |
| 15 | CRDB BANK PLC |
| 16 | DCB COMMERCIAL BANK PLC |
| 17 | DIAMOND TRUST BANK TANZANIA LTD |
| 18 | E.A CAPITAL LIMITED |
| 19 | ECOBANK TANZANIA LIMITED |
| 20 | EQUITY BANK (TANZANIA) LIMITED |
| 21 | EXIM BANK (TANZANIA) LTD |
| 22 | FIMCO LIMITED |
| 23 | FIRST NATIONAL BANK TANZANIA LIMITED |
| 24 | GUARANTY TRUST BANK (TANZANIA) LTD |
| 25 | HABIB AFRICAN BANK LIMITED |
| 26 | I AND M BANK (T) LTD |

| | |
|---|---|
| 27 | INTERNATIONAL COMMERCIAL BANK |
| 28 | KCB BANK TANZANIA LIMITED |
| 29 | MAENDELEO BANK PLC |
| 30 | MKOMBOZI COMMERCIAL BANK PLC |
| 31 | MWALIMU COMMERCIAL BANK |
| 32 | NATIONAL BANK OF COMMERCE LTD |
| 33 | NATIONAL MICROFINANCE BANK PLC |
| 34 | NCBA BANK TANZANIA LIMITED |
| 35 | OPTIMA CORPORATE FINANCE |
| 36 | ORBIT SECURITIES CO LTD |
| 37 | RASILIMALI LIMITED |
| 38 | SMART STOCK BROKERS (T) LTD |
| 39 | SOLOMON STOCKBROKERS LIMITED |
| 40 | STANBIC BANK TANZANIA LIMITED |
| 41 | STANDARD CHARTERED BANK TANZANIA LTD |
| 42 | TANZANIA AGRICULTURAL DEVELOPMENT BANK LIMITED |
| 43 | TANZANIA POSTAL BANK |
| 44 | TANZANIA SECURITIES LIMITED |
| 45 | THE PEOPLE’S BANK OF ZANZIBAR LIMITED |
| 46 | UBL BANK (TANZANIA) LIMITED |
| 47 | UNITED BANK FOR AFRICA (T)LTD |
| 48 | VERTEX SECURITIES LTD |
| 49 | VICTORY FINANCIAL SERVICES LTD |
| 50 | YETU MICROFINANCE BANK PLC |
| 51 | ZAN SECURITIES LTD |

Benki kuu ya Tanzania inayo haki ya kufanya marekebisho kuhusu taratibu na mwongozo huu wakati wowote itakapokuwa ni lazima kufanya hivyo.

**IDARA YA MASOKO YA FEDHA**
**KURUGENZI YA MASOKO YA FEDHA**
**MEI 2021**

## FAHIRISI

**Akaunti ya Dhamana:** Akaunti inayotunzwa na Idara ya Masoko ya Fedha kwa ajili ya kuhifadhia kumbukumbu ya Dhamana zitolewazo kama dhamana kwa ajili ya mikopo.

**Dhamana ya mkopo:** Dhamana za Serikali ambazo hutolewa kwa ajili ya kudhamini mkopo na zinabakia kuwa hivyo kwa kipindi chote cha mkopo.

**Akaunti ya umiliki:** Hii ni akaunti inayohifadhi kumbukumbu za wawekezaji wote wa Dhamana za Serikali.

**Akaunti ya pamoja:** Hii ni akaunti inayosimamiwa na Idara ya Masoko ya Fedha ya Benki Kuu ya Tanzania ili kuwawezesha wawekezaji kupata taarifa sahihi kuhusu viwango vya Dhamana za Serikali wanazozimiliki katika muda husika.

**Bei ya chini na ya mwisho katika kuuza Dhamana:** Hii ni bei ya chini na ya mwisho inayokubalika katika kuuza na kuhakikisha kiwango cha Dhamana kilichotolewa kinamalizika.

**Dhamana za Serikali:** Hizi ni Dhamana za muda mfupi na za muda mrefu zinazotolewa kwa mujibu wa sheria ya Mikopo na Dhamana ya mwaka 1974 iliyo rekebishwa mwaka 2004.

**Dalali:** Mtu anayewaunganisha wanunuzi na wauzaji ili wafanye biashara. Mara nyingi huwatoza ushuru.

**Kuiva kwa Dhamana:** Hii ni tarehe ambayo Dhamana za Serikali zinalipwa baada ya kumalizika kwa kipindi cha uwekezaji kilichokubalika awali.

**Mfumo wa malipo:** Ni mfumo wa kubadilishana na kufanya malipo bila ya kutumia uhamishaji wa nyaraka au vyeti.

**Mawakala:** Haya ni mabenki ya biashara ambayo yamepewa leseni na Benki Kuu pamoja na taasisi ambazo zimesajiliwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA). Mabenki na taasisi hizi huwekeza katika Dhamana za Serikali kwa ajili yao binafsi au kwa niaba ya wateja wao.

**Mfumo mkuu wa hifadhi:** Hizi ni kumbukumbu zilizohifadhiwa kwa njia ama ya kawaida au kwa kutumia mfumo wa kompyuta. Mfumo huu ambao unasimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania huhifadhi kumbukumbu zote zinazohusu umiliki wa Dhamana za Serikali

**Mauziano ya Dhamana za Serikali nje ya soko maalumu (OTC):** Huu ni utaribu wa kuuza Dhamana kwa njia ya makubaliano kati ya muuzaji na mnunuzi bila kupitia kwenye masoko maalumu.

**Namba ya malipo:** Hii ni namba inayotumika na mabenki katika kutuma malipo ya Dhamana zilizonunuliwa kwenye mnada "bid code"

**Soko la awali:** Hili ni soko linalohusika na matoleo mapya ya Dhamana za Serikali kabla ya kumilikiwa na wawekezaji binafsi.

**Soko:** Uuzaji wa Dhamana za Serikali kati ya wanunuzi na wauzaji wa Dhamana za Serikali katika soko la wazi bila kuingiliwa na Benki kuu ya Tanzania.

**Siku ya malipo ya manunuzi:** Ni siku ambayo Dhamana za Serikali hutolewa kwa washindi baada ya kulipia kiasi kinachotakiwa.

**Siku Dhamana inapoiva:** Ni siku ambayo Dhamana za Serikali zikiwepo zile za muda mfupi na za muda mrefu zinapoiva kwa malipo ya mwisho.

**Taarifa ya akaunti:** Hii ni taarifa inayotokana na akaunti ya pamoja inayowahusu wawekezaji ikionyesha hali halisi ya malipo yaliyofanyika na kiasi kilichopo katika akaunti za wawekezaji.

**TISS:** Huu ni mfumo wa malipo yanayofanywa moja kwa moja kwa njia za kielektroniki. Mfumo huu huwezesha malipo ya Dhamana za Serikali kufanyika kwa urahisi.

**Thamani ya Dhamana:** Thamani halisi ya Dhamana itakayolipwa pale Dhamana itakapoiva

**Tarehe ya thamani:** Ni tarehe ambayo uuzaji au ununuzi wa Dhamana unafanyika.

**Utaratibu wa KUWEKA Kumbukumbu:** Huu ni utaratibu wa kielektroniki wa kupitisha na kuhifadhi kumbukumbu pasipo kuhusisha ubadilishanaji wa hati au shahada zozote.

**Wawekezaji wa moja kwa moja:** Hawa ni wawekezaji wasiokuwa Madalali ambao huwekeza kiasi kisichopungua shilingi milioni tano kwa wakati mmoja.

**MAULIZO YOTE YAWASILISHWE KWA:**

Meneja
Idara ya Masoko ya Fedha
Benki Kuu ya Tanzania,
S.L.P 2939
Dar-es-Salaam
Simu: 022 – 2234494-97
Simu: 022 – 22333529
Nukush: 022-2234049

Mkurugenzi wa Tawi,
Benki Kuu ya Tanzania,
S.L.P. 3043
Arusha,
Simu: 027 – 2545541-3
Nukushi: 027 – 2545444/2548722

Mkurugenzi wa Tawi,
Benki Kuu ya Tanzania,
S.L.P 1362
Mwanza,
Simu: 028 – 2500313/2500315-7
Nukushi: 028 – 2500277

Mkurugenzi wa Tawi,
Benki Kuu ya Tanzania
P.O Box 1203
Mbeya
Simu: 025 – 2503321-3
Nukushi: 025 – 2502844/2502602

Mkurugenzi wa Tawi,
Benki Kuu ya Tanzania S.L.P 2303
Dodoma,
Simu: +255 222232506
Nukushi:

Mkurugenzi wa Tawi,
Benki Kuu ya Tanzania S.L.P 568
Zanzibar
Simu: 024 – 2230803/2238234
Nukushi: 024 – 2230415

**KIAMBATANISHO I**
**Mfano: Uitishaji Zabuni**

## TREASURY BILLS AUCTION NUMBER 1083: INVITATION TO TENDER ON 11th MAY 2021

The Bank of Tanzania on behalf of the Government of the United Republic of Tanzania invites applications through Central Depository Participant (CDP) to tender for Treasury Bills of which terms and conditions are as follows:

| | | |
|---|---|---|
| **Issuer** | United Republic of Tanzania | |
| | **Competitive** | **Non-Competitive** |
| **Maturities/Amount** | 35 days up to TZS 1,000 Million | 100 Million |
| | 91 days up to TZS 1,700 Million | 100 Million |
| | 182 days up to TZ 3,000 Million | 100 Million |
| | 364 days up to TZS71,000 Million | 220 Million |
| **Auction date** | **Tuesday 11th May 2021** | |
| **Procedure for bidding** | **Bids will be submitted online through Central Depository Participants (CDPs) and the process will be closed at 11.00 a.m. on the auction date** | |
| **Price per TZS 100** | **To be quoted at a discount to four (4) decimal places** | |
| **Minimum bid size** | TZS 500,000 in multiples of TZS 10,000 | |
| **Auction results** | Auction results shall be made available on the Bank's Website and at Central Depository Participants' offices immediately after the auction | |
| **Settlement date** | **Wednesday 12th May 2021 (T+1)** | |
| **Form of issuance** | Book entry system | |

| | |
|---|---|
| **Redemption date** | Redemption dates: 35 – Day 16th June 2021<br>91 – Day 11th August 2021<br>182 – Day 10th November 2021<br>364 – Day 11th May 2022 |
| **Tax** | Interest income is subject to 10% withholding tax |
| **Currency** | Tanzania Shilling (TZS) |
| **Defaulters** | Successful bidders who fail to honor their obligations on time will be disqualified from participating in the subsequent auctions for a minimum period of one (1) month |

**The Bank of Tanzania reserves the right to accept or reject any or all applications.**

For further details, please contact Financial Markets Department, Bank of Tanzania, 2 Mirambo Street,11884 Dar es Salaam, P.O. Box 2939, Dar es Salaam (Tel: +255222234494-97, Fax: +255222234217), E-mail: info@bot.go.tz, Web: https://www.bot.go.tz

**Kiambatisho II**
**CDS/FORM/03**

**BID APPLICATION FORM**
**TO PARTICIPATE IN THE AUCTION OF SECURITIES**

| |
|---|
| **Authorised Dealer Name:……………………………………………** |

| |
|---|
| **CDS SEC A/C:……………………………………………………………….** |

| |
|---|
| **Account Name:……………………………………………………………….** |

**Manager Financial Markets**
**Bank of Tanzania**
**P.O. Box 2939**
**Dar es Salaam** **Date:……………….**

| |
|---|
| **Security Type:** |

**Issuer: Government of Tanzania**

**Auction Date…………… Maturity Period………Days/Years**

I/We tender for Government Securities with the following specifications:

**Amount of Tender** **Price per 100 shillings**
(Face Value) (Two Decimal places for T-Bills or Four Decimal places for T-Bonds)

**(1) Tshs …………………** **@………….**
**(2) Tshs ………………** **@…………..**
**(3) Tshs……………….** **@…………..**
**(4) Tshs……………….** **@…………….**

In accordance with the terms of the call for tenders for Government securities, I / We hereby agree to pay through TISS-DVP for the total, amount that shall be allotted at the price per hundred shillings

……………. ……………… …………………
Date Authorised Signature Authorised Signature

**KIAMBATANISHO III**

**CDS/FORM/04**

## CDS Form 03: GOVERNMENT SECURITIES TRANSFER FORM

(To be submitted in duplicate to the Manager Financial Markets)

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | **Authorized Dealers:** | | | | | | | | |
| | **1.** Selling Dealer | **Name** | | | | | | | |
| | | **CDS SEC. A/C** | | | | | | | |
| | **2.** Buying Dealer | **Name** | | | | | | | |
| | | **CDS SEC. A/C** | | | | | | | |
| 2 | **Transacting on behalf of the client:** | | | | | | | | |
| | **1.** Seller | **Name** | | | | | | | |
| | | **CDS SEC. A/C** | | | | | | | |
| | **2.** Buyer | **Name** | | | | | | | |
| | | **CDS SEC. A/C** | | | | | | | |
| 3 | **Subject:** | | | | | | | | |
| | **1.**Nature of Transaction* | | | | | | | | |
| | **2.**Bond no | | | | | | | | |
| | **3.**Bond Auction no. | | | | | | | | |
| | **4.**Bond Holding no. | | | | | | | | |
| | **5.**Treasury Bills Auction no. | | | | | | | | |
| | **6.**Treasury Bills Holding no. | | | | | | | | |
| | **7.**Face Value | | | | | | | | |
| | **8.**Price | | | | | | | | |
| | **9.** Discounted Amount | | | | | | | | |
| 4 | **Delivery Instructions:** | | | | | | | | |
| | **1. CDS SEC. A/C** | **Debit Account No** | | | | | | | |
| | | **Credit Account No** | | | | | | | |
| | **2.** Value Date (**DD-MM-YYYY)** | | | | | | | | |

| | | |
|---|---|---|
| 5 | **Confirmation:** | |
| | 1. Authorized Signatory | |
| | 2. Authorized Signatory | |

**KIAMBATANISHO IV**

**CDS/FORM/05**

**Manager Financial Markets**
**Bank of Tanzania**
**P.O. Box 2939**
**Dar Es Salaam   Date: ……………..…………………**

Name of the CDS securities account on which the lien is being created:

…………………………………………………………………………………
…….. CDS securities a/c. number on which the lien is being created

| | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|

Name of the CDS securities account holder to benefit from the lien:
……………………………………………………………………………….
CDS securities a/c. number of the CDS member to benefit from the lien

| | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|

Value date of the lien (DD/MM/YYYY):___/_______/_______

Holding number of the CDS securities to be placed under lien: _______

Maturity date of the issue (DD/MM/YYYY):_______/_______/______

Maturity date of the lien (DD/MM/YYYY):_/_______/_______

Face Value of lien: | TZS |

Value in words:.........................................................................

**Instructions for disposing of the lien:**

In the event that CDS securities posted as collateral mature before the lien has been released by the creator of the lien, then the face value of the affected CDS securities will automatically be credited to the settlement bank of the beneficiary of the lien.

**Date** ____________________ **Authorized Signature** ____________________ **Authorized Signature**

---

**For Official Use Only**

**Verified By:____Sign___Date__________**
**Approved By:__Sign___Date__________**
**Remarks: _____**

**KIAMBATANISHO V**

**CDS/FORM/06**

(To be submitted in duplicate and delivered to the Manager Financial Markets)

**Manager Financial Markets Bank of Tanzania**
**P.O. Box 2939**
**Dar es Salaam** **Date: …………..…………………**

Name of the CDS securities account on which the lien is being released:

………………………………………………………………………………… …….. CDS securities a/c. number to be credited on release of the lien:

| | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | | | | | |

Name of the CDS securities account holder releasing the lien:
……………………………………………………………………………….
CDS securities a/c. number on which the lien is being released:

| | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | | | | | |

Value date of the lien release (DD/MM/YYYY):____/_______/_______

Holding number of the CDS securities to be released from lien:_______

Maturity date of the issue (DD/MM/YYYY):_______/_______/_______

Maturity date of the lien (DD/MM/YYYY):_/_______/_______

Face Value of the lien release: TZS:

Value in words: ........................................................

| ------------------ | ------------------------ | ----------------------- |
|---|---|---|
| **Date** | **Authorized Signature** | **Authorized Signature** |

**Verified By:__________Sign_____Date______________**

**Approved By:_______Sign______Date**

**Remarks:_____________**

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na Idara ya Masoko ya Fedha,**

Benki Kuu ya Tanzania,

Mtaa wa Mirambo Namba 2,

S.L.P. 2939 Dar es Salaam.

Namba za simu 2233481-90, 2233473-4,

Nukushi 2234049 na

Tovuti: www.bot.go.tz

MFANO